**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE**
**SHULE YA SEKONDARI UKEREWE**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI UKEREWE 2025

**MZAZI/ MLEZI WA.......................................................................................................**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na **Shule ya Sekondari Ukerewe**. Shule inapatikana mkoa wa Mwanza, wilaya ya Ukerewe, kata ya Kagunguli, kijiji cha rwesabi. Shule yetu ni ya BWENI na ni ya wasichana pekee.

## MTAALA WA SHULE

Shule inafundisha kwa kutekeleza mtaala wa serikali unaotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Shule ya sekondari Ukerewe ina matarajio na malengo makubwa ya kuzalisha wanafunzi wenye umahili mkubwa hasa katika masomo ya sayansi na Sanaa mbalimbali ili kumwezesha mwanafunzi kumudu ushindani katika ajira, fursa na ujasirianali kwa maendeleo ya taifa letu.

## MAHITAJI MUHIMU KWA MWANAFUNZI

### A’ VIFAA VYA TAALUMA

1. Counter books zisizopungua kumi (10) na madaftari madogo tisa (09) ya msomi
2. Rula moja, penseli za kutosha, kalamu za wino mweusi au bluu, file la kuhifadhia mitihani na mkebe wa hisabati (mathematical set)
3. Rimu moja ( mchango huu wa rimu umepitishwa na kikao cha wazazi)
4. Begi la kubebea madaftari

### B’ VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI

5. Sanduku la nguo la chuma (trunker)
6. Vyombo vya chakula; sahani, kijiko, kikombe na bakuli
7. Godoro (futi 2.5/ mbili na nusu), Net ya kuzuia mbu (iwe ya rangi ya bluu bahari ya duara).
8. Mashuka mawili (02) (moja rangi ya pink na moja la rangi ya blue)
9. Mto,taulo na khanga / kitenge kipande moja.
10. Taulo (sanitary pads) za kutosha
11. Nguo moja kulalia na nguo za ndani za kutosha.
12. Dawa ya meno,mswaki,toilet paper,kiwi,brush ya viatu,mafuta ya kupaka na sorata ya kuchaji juani.
13. Sabuni za mche, za unga na kopo la kuogea pamoja na sabuni ya kuogea
14. Ndoo mbili (02) za mafuta na dishi moja (01) kwa ajilki ya matumizi binafsi na matumizi ya shule.
15. Jozi moja ya viatu vya ngozi nyeusi vya darasani visivyo na kisigino kirefu wala urembo, vya kufunga na kamba.

16. Kandambili, sendals za kufunga nyuma na sio za kuchomeka na raba nyeupe za mchezo jozi moja(yebo yebo haziruhusiwi kabsa)
17. Track suit moja na tshirt mbili, **zitapatikana shuleni** kwa gharama ya tsh 44,000/ zikiwa na nembo zake.
18. Blanketi moja.
19. Uniform (Sare) za shule
    - Sketi ya dark green **(kijani ya jeshi)** (skirt iwe ya rinda box,iwe na rinda kubwa mbele na nyuma. Na marinda ya pembeni yawe mawili) kipande cha sampuli ya kitambaa utapewa shuleni.
20. Shati nyeupe mbili (02) zenye mikono mifupi na socks ndefu nyeupe (pea tatu)
21. Sweater moja rangi ya dark blue

NB: Mzazi hakikisha unaweka alama ya kuonekana kwenye vifaa vya mwanao kama ndoo, nguo za ndani,mashuka n.k kuepuka mtoto kuchanganya vitu vyake na vya wenzake.

## TAALUMA, MIHULA YA SHULE NA LIKIZO.

Mwanafunzi anatakiwa kusoma masomo yafuatayo: Biology, Physics, Chemistry, Basic Mathematics, Civics, English, Kiswahili, History na Geograohy pamoja na masomo mengine kulingana na mabadiriko ya mtaala wa elimu.

- **lUGHA YA MAWASILIANO MUDA WOTE WANAFUNZI WAWAPO SHULENI NI KIINGEREZA, ISIPOKUA WAKATI WA SOMO LA KISWAHILI TU.**
- Mwanafunzi anapaswa kusoma kwa bidii na kupata ufaulu wa alama kuanzia **65 yaani wastani wa B** kwa mazoezi na mitihani yote atakayofanya pindi awapo shuleni**,(mitihani ya ndani na nje ya shule). Kufeli mitihani ni utovu wa nidhamu hivyo mwanafunzi atapewa adhabu.**
- Shule inafuata na kuzingatia mihula inayotolewa na wizara ya elimu.

## USAFI

- Mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wake binafsi na mazingira ya shule. Kauli mbiu yetu ya kimazingira ni **"Keep Our School Environment Clean For Better Learning".**
- Mwanafunzi anatakiwa kufuata utaratibu wa usafi kama atakavyoelekezwa na idara ya usafi na mazingira shuleni.
- Mwanafunzi

## VIFAA VISIVYORUHUSIWA SHULENI.

- Simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu (mfano: charger, laini, betri za simu n.k)
- Taa za aina zote za kuchaji kwenye umeme
- Heater za kuchemsha maji
- Camera
- Radio aina zote
- Vifaa vya michezo vya umeme (electronic games)
- Marashi, vipodozi hasa kwa wasichana
- Silaha kama visu, mishale, panga na chupa.

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.

Shule hii inamilikiwa na serikali. pia inaongozwa kwa kufuata misingi na maadili ya kitaifa. Mwanafunzi awapo shuleni anapaswa kufuata taratibu zote zilizowekwa kadiri ya ratiba ya shule.

1. Wanafunzi wote watapaswa kufuata na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za shule. Kinyume chake adhabu zitatolewa ikiwa ni pamoja na kupewa onyo la kawaida,kusimamishwa shule kwa muda au kufukuzwa kabisa.
2. Mwanafunzi anatakiwa kujali na kuheshimu mipango yote ya taaluma kwani ndio iliyomleta hapa shuleni.
3. Ni marufuku kupiga kelele au kuleta usumbufu wa aina yoyote ile ndani ya eneo la shule.
4. Mwanafunzi atatakiwa kuwa darasani muda wote wa vipindi, kama sivyo atatakiwa kuwa na ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa darasa/mwalimu wa zamu.
5. Mwanafunzi analo jukumu la kutunza mali zake na za shule
6. Mwanfunzi ana jukumu la kujali utu na ubinadamu wake na wa wenzake, pia awe mkweli na kumuogopa Mungu.
7. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote darasani, kufanya majaribio,mazoezi na kufanya mitihani ya ndani na nje ya wilaya kama ratiba na utaratibu utakavyo onyesha
8. Mwanafunzi haruhusiwi kuleta au kuletewa chakula kutoka nje ya shule

## MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- Wizi
- Mapenzi ya aina yote
- Uasherati, ubakaji, ushoga na usagaji.
- Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
- Uvutaji bangi, mirungi, sigara
- Makosa ya jinai kama kuua
- Kupiga au kupigana
- Kusema uongo
- Kudharau wimbo wa shule na alama za shule, kudharau wimbo wa taifa na alama za taifa
- Kutoa mimba, kusababisha mimba nje na ndani ya shule
- Kuoa au kuolewa
- Kukataa au kugomea adhabu
- Utoro
- Kuendesha mgomo,kuchochea au kuongoza vurugu za kuhatarisha amani na usalama wa watu na mali zao
- Udanganyifu wakati wa mitihani
- Udhalilishaji wa kijinsia kwa yeyote
- Kutumia lugha chafu kwa wanafunzi na wafanyakazi wote
- Kubaguana

## MAELEKEZO MUHIMU SHULE

- Kikao cha wazazi kitafanyika mara mbili kwa mwaka.Tarehe itategemea kalenda ya shule. Siku hiyo wazazi wanaweza kusalimiana na watoto wao.

- wazazi wakija shule **hawaruhusiwi kuleta chakula cha aina yoyote** ile shuleni. Kinyume na hapo mtoto ataachishwa shule kwa kosa la kuletewa chakula toka nje ya shule.
- Aidha mzazi/mlezi anayetambulika anaweza kufika shuleni kumsalimia mtoto kwa ridhaa ya Mkuu wa shule/Makamu mkuu wa shule tu.
- Mwanafunzi lazima awe na bima ya afya
- Endapo mwanafunzi atalazimika kupata matibabu nje ya shule Pamoja na kulazwa mzazi ataghamia na kumuuguza mwanae.
- Mawasiliano yote ya mwanao tumia namba zifatazo 0755650134 au 0753544864 mzazi atakayetumia mawasilino tofauti na namba hizo shule haitahusika kwa lolote.
- Wanafunzi wenye maagonjwa ya kudumu mfano pumu,sikoseli,kifafa waje na ;
  1. Cheti cha dakdari kutoka hospitali ya wilaya au mkoa
  2. Aje dawa za kumsaidia mfano spray kwa wenye pumu, foliki aside na dawa za kuongeza damu. Vilevile mzazi atakapopewa taarifa za ugonjwa wa mwanae afike shuleni mara moja vinginevyo mwanafunzi atarudishwa nyumbani.
  3. Aje mti mmoja wa kivuli kwa ajili kuboresha mazingira ya shule.


**MWISHO.**

Tutaanza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza tarehe 04/01/2025 kuanzia saa 02:00 asubuhi hadi 9:30 arasili

Nakutakia maandalizi mema ya kujiunga na jamii ya watu wa **Ukerewe Sekondari** kwa elimu bora na malezi bora.

**MOTTO WA SHULE:** ***"EDUCATION AND KNOWLEDGE FOR SERVICE"***

**KARIBU SANA**



**REBECA SIMON LYANGA**
**MKUU WA SHULE**
**0754648787**

